

HALMASHAURI YA WILAYA KILINDI



TANGAZO KWA WAFANYABIASHARA WADOGO

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi inawatangazia wananchi wote wa Wilaya ya Kilindi kuwa Ofisi ya Rais TAMISEMI imeanza zoezi la kutoa vitambulisho vipyta vya wajasiliamali kufuatia vitambulisho vilivyo tolewa 2020 kumalizika muda wake.

Hivyo vitambulisho vinavyotolewa mwaka huu wa 2021 vimefanyiwa Maboresho ili kuongeza taarifa muhimu za mwombaji ambazoni *Jina kamili, Picha, Eneo la makazi, Ukomo wamatumizi yakinatalisho pamoja na Jinsia ya mwombaji*. Vitambulisho hivi vilivyo boreshwa vinatoa fursa kwa wafanyabiashara wadogo na watoa huduma ndogo kupata mikopo kuitia taasisi mbalimbali za fedha hapa nchini.

UTARATIBU MPYA WA KUPATA KITAMBULISHO CHA MJASILIAMALI

A: KWA NJIA YA KUTUMIA KIVINJARI (WEB BROWSER)

1. Tembelea tovuti ya ofisi ya rais TAMISEMI ambayo ni www.tamisemi.go.tz chagua sehemu ilio andikwa **Machinga Online Registration**.
2. Weka namba yakinatalisho cha Taifa au leseniyaudereva au bofya sina namba ya kitambulisho kama huna.
3. Kama ulitumia kitambulisho taarifa zako zitakuja zenyewe kutoka katika mfumo lakini kama hujatumia kitambulisho utatakiwa kujaza taarifa zako binafsi kasha chagua wasilisha.
4. Hakiki taarifa zako kama ni sahihi kasha Chagua *Endelea*.
5. Baada ya hapo ombi lako litapokelewa nakupewa namba, na kili namba hiyo kwani itahitajika wakati wa kufatilia maombi yako.

B: KWA NJIA YA KUTUMIA "APP" YA SIMU JANJA

1. Nenda kwenye *Google Play Store* ya simu janja yako nakishapakua application "*Official Machinga app*".
2. FunguaApp uweke namba ya simu kasha chagua "*Ombakitambulisho*" kasha Bofya *Endelea*.
3. Chagua kitambulisho ulicho nacho kama huna basi Bofya "*Sina Kitambulisho*".

4. Kama huna kitambulisho chagua "*pigapicha*" au chagua picha ili yopo katika simu yako kwa ajili ya kitambulisho.
5. Kama ulitumia kitambulisho taarifa zako zitajazwa zenyewe kutoka kwenye mfumo, kama hujatumia kitambulisho jaza taarifa zako binafsi.
6. Chagua Mkoa, Wilaya, Eneo la biashara kasha chagua Aina ya Biashara, Makadirio ya mauzo kasha chagua "*Endelea*".
7. Hakiki Taarifa zako kasha Bonyeza "*Endelea*", Ombi lako litapokelewa nakupewa namba, kasha nakili namba hiyo ambayo itatumika wakati wa kufatilia maombi yako.

GHARAMA ZA KITAMBULISHO

Gharama za kitambulisho ni Shilingi za kitanzania 20,000/= tu ambazo zitalipwa kupitia mfumo wa malipo waserikali (GEPG) kwa namba ya malipo (**Control Number**) ambayo mfanyakia shara Mdogo ama mto huduma mdogo atapatiwa kupitia simu yake baada ya kukamilisha Usajili na atatakiwa kulipia kwa kutumia Simu yake ya *M-PESA, Airtel Money* nk au Benki au Wakalawa Benkiyoyote.

UGAWAJI WA VITAMBULISHO

Ofisi ya Meneja wa Mamlaka ya Mapato (TRA) Mkoa itavipeleka vitambulisho katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa nayo itavikabidhi katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya.
 Ofisi ya Mkuu wa Wilaya itavikabidhi vitambulisho hivyo katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri za Wilaya, Ambapo Ofisi ya Halmashauri kupitia Kitengo cha Biashara ndicho kitahusika kugawa Vitambulisho kwa wahusika.

ANGALIZO

Kwa waombaji ambao watakao shindwa kutumia njia ya Simu Janja au Tovuti ya TAMISEMI wanaweza kuwasilisha maombi yao kupitia ofisi maalumu za TAMISEMI zilizoko karibu yao.

NB:-Kwa Kilindi unaweza kuwasiliana na:

Afisa Biashara (W) 0784 591 988 / 0623 389 038

Afisa TEHAMA (W) 0621 083 341

kwa msaada wa kufanya maombi ya kitambulisho cha Mjasiriamali


Gracian M. Makota
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
KILINDI

*MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
KILINDI*